JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA FAMASI**

# MABADILIKO YA TAREHE YA MITIHANI YA TAALUMA KWA WAHITIMU WA KOZI ZA FAMASI

**DODOMA: 21 Oktoba, 2025**

Mnamo tarehe **22 Agosti, 2025** Ofisi ya Msajili ilitoa tangazo kupitia tovuti ya Baraza lililohusu matokeo ya mitihani ya taaluma iliyofanyika Julai, 2025 na tarehe ya mitihani ya taaluma inayofuata kwa wahitimu wa kada za famasi wanaohitaji kusajiliwa na Baraza kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Famasi Sura 311.

Ofisi inapenda kuwataarifu wahitimu waliowasilisha maombi, kuwa tarehe ya kufanya mitihani hiyo imesogezwa mbele na itafanyika tarehe **26 - 28 Novemba, 2025** badala ya tarehe **12 - 14 Novemba, 2025** kama ilivyotangazwa awali. Vilevile Ofisi inapenda kuwafahamisha kuwa inaendelea kupitia na kuidhinisha maombi ya mitihani yaliyowasilishwa ili kuwezesha wahitimu kupata namba ya mitihani.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe info@pc.go.tz/ registration@pc.go.tz au Simu: 0736222503/0736222515.

**Imetolewa na;**
**MSAJILI**
**BARAZA LA FAMASI**
**S.L.P 1277, Dodoma**